**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA AFYA**

# TAARIFA KWA UMMA KUHUSU KUANZA MAFUNZO YA WAHUDUMU WA AFYA NGAZI YA JAMII KWENYE MIKOA 11

**19 Septemba, 2024, Dar Es Salaam.**

**Ndugu Wananchi;**

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia **Wizara ya Afya** na **Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa** (**OR -TAMISEMI**) inatekeleza **Mpango Jumuishi wa Wahudumu wa Afya Ngazi ya Jamii** nchini. Kupitia Mpango huu, Serikali imeweka utaratibu wa kuwapata Wahudumu wenye sifa stahiki, kutoa mafunzo kwa wahudumu hao ili waweze kutekeleza afua Jumuishi za Afya, Lishe na Ustawi wa Jamii.

**Ndugu Wananchi;**

Katika kutekeleza Mpango huu, **Wizara** inatangaza kuwa imeanza kutekeleza **Mpango huu katika Halmashauri ishirini na tatu (23) ndani ya Mikoa 11** kwa awamu hii ya kwanza. **Mikoa hiyo ni Geita, Pwani, Tanga, Songwe, Mbeya, Lindi, Tabora, Kagera, Njombe, Kigoma na Ruvuma.**

**Ndugu Wananchi;**

Utekelezaji wa Mpango huu kwenye Mikoa iliyoainishwa ulianza kwa kutoa tangazo la nafasi za Wahudumu wa Afya Ngazi ya Jamii kuomba nafasi hizo na kufuatiwa na zoezi la jamii ya maeneo husika kuchagua Wahudumu wenye sifa stahiki. Wahudumu wawili wanahitajika, yaani Mwanaume na Mwanamke kwa kila Kitongoji/Mtaa.

Zoezi la kuwachagua Wahudumu wa Afya Ngazi ya Jamii lilifanyika kati ya tarehe **08/06/2024 hadi 25/07/2024** kwenye Halmashauri ishirini na moja (21) katika Mikoa kumi na kwa Mkoa wa Ruvuma zoezi linaendelea.

**Ndugu Wananchi;**

**Jumla ya Wanajamii Elfu Thelathini na Moja, Mia Mbili Sabini na Tano (31,275)** walijitokeza kuomba nafasi hizi. Jumla ya waombaji **Elfu Ishirini na Moja, Mia Tano Sabini na Nne (21,574)** walikidhi vigezo na kuingia katika hatua ya kuchaguliwa ndani ya jamii. Mchakato huu ulihusisha jumla ya Mitaa **Elfu Moja na Arobaini na Nne (1,044), Vijiji Mia Saba Hamsini na Nne (754) na Vitongoji Elfu Tatu Mia Nane Hamsini na Tatu (3,853).** Baada ya zoezi la mchujo (shortlisting) na uchaguzi kupitia mikutano ya jamii, **jumla ya Wahudumu wa Afya Ngazi ya Jamii Elfu Tisa, Mia Nne Tisini Na Mbili (9,492) walichaguliwa** na kwa Mkoa wa Ruvuma jumla ya Wahudumu wa Afya Ngazi ya Jamii Elfu Moja, Mia Mbili, Ishirini na Saba 1227 watachaguliwa. Hivyo kuwa na **Wahudumu wa Afya Ngazi ya Jamii, Kumi na Moja Elfu, Mia Tano, Kumi na tano (11515)** kama ifuatavyo;-

| NA | MKOA | HALMASHAURI | IDADI YA CHWs | JUMLA |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Mkoa wa **Geita** | *Halmashauri ya Mji Geita* | 224 | 939 |
| | | *Halmashauri ya Wilaya ya Bukombe* | 715 | |
| 2 | Mkoa wa **Pwani** | *Halmashauri ya Mji Kibaha* | 146 | 491 |
| | | *Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji* | 345 | |
| 3 | Mkoa wa **Tanga** | *Halmashauri ya Jiji la Tanga* | 362 | 482 |
| | | *Halmashauri ya Mji wa Handeni* | 120 | |
| 4 | Mkoa wa **Songwe** | *Halmashauri ya Wilaya ya Ileje* | 632 | 774 |
| | | *Halmasahuri ya Mji Tunduma* | 142 | |
| 5 | Mkoa wa **Mbeya** | *Halmashauri ya Jiji la Mbeya* | 374 | |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | na *Halmashauri ya Wilaya ya Busekelo* | 474 | 848 |
| 6 | Mkoa wa **Lindi** | *Halmashauri ya Manispaa ya Lindi* | 730 | 2,616 |
| | | *Halmashauri ya Wilaya ya Mtama* | 1,014 | |
| | | *Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa* | 872 | |
| 7 | Mkoa wa **Tabora** | *Halmashauri ya Manispaa ya Tabora* | 506 | 886 |
| | | *Halmashauri ya Mji wa Nzega* | 380 | |
| 8 | Mkoa wa **Kagera** | *Halmashauri ya Mji Bukoba* | 717 | 849 |
| | | *Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo* | 132 | |
| 9 | Mkoa wa **Njombe** | *Halmashauri ya Mji Makambako* | 219 | 589 |
| | | na *Halmashauri ya Mji wa Njombe* | 370 | |
| 10 | Mkoa wa **Kigoma** | *Halmashauri ya Wilaya ya Buhigwe* | 308 | 1,018 |
| | | *Halmashauri ya Wilaya ya Kakonko* | 710 | |
| **11** | Mkoa wa **Ruvuma** | *Halmashauri ya Mji wa Songea* | 285 | 1227 |
| | | *Halmashauri ya Wilaya ya Songea* | 942 | |
| | **JUMLA** | | | **11515** |

***Mafunzo haya yatakuwa yanatolewa kwa awamu. Orodha ya majina ya Wahudumu Waliochaguliwa kujiunga na mafunzo kwa awamu ya kwanza na Vyuo walivyopangiwa inapatikana katika Tovuti ya; Wizara ya Afya,***

***OR – TAMISEMI, Ofisi za Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya na Ofisi za Wakurugenzi wa Halmashauri husika.***

**Ndugu Wananchi;**

Baada ya kukamilisha zoezi la kuwachagua Wahudumu kwa awamu ya kwanza, Wizara ya Afya inapenda kuutaarifu umma kwamba maandalizi ya mafunzo rasmi ya kuwajengea uwezo Wahudumu yamekamilika na mafunzo yataanza rasmi mnamo Tarehe **30 Septemba, 2024.**

Mafunzo yatatolewa katika **Vyuo vya Afya vya Kada za Kati** kwa kipindi cha **miezi sita (06**). Miezi mitatu ya awali, mafunzo yatatolewa kwa njia ya nadharia na miezi mitatu iliyobaki mafunzo yatakua kwa njia ya vitendo kwenye maeneo wanayotoka ili kuongeza umahiri kwa Wahudumu kutekeleza kwa uhalisia kile walichojifunza. Mafunzo hayo yatatolewa katika Vyuo vilivyoainishwa kwenye Halmashauri anayotoka Mhudumu au maeneo ya jirani.

**Ndugu Wananchi;**

Wizara ya Afya inatoa pongezi kwa Wahudumu wote waliochaguliwa miongoni mwa Wanajamii. Aidha, Wizara inatoa rai kwa Wahudumu waliochaguliwa kufika kwa wakati kwenye Vyuo walivyopangiwa na kufuata taratibu zote za mafunzo kama zitakavyotolewa na Vyuo husika. Vilevile wanajamii wote wanaombwa kushirikiana kwa karibu na Wahudumu mara baada ya kuhitimu mafunzo yao na kurudi kutumikia jamii. Natoa rai kwa jamii tuendelee kuwa na usalama wa utambuzi ni muhimu kwa Wanajamii kutambua Wahudumu wa Afya Ngazi ya Jamii watakaowahudumia ni wale ambao waliwachaguliwa na kuwapitishwa kama Jamii husika.

Hizi ni juhudi zinazoendelea kufanywa na Serikali ya Awamu ya Sita, chini ya Uongozi wa **Rais Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan** ambaye ameonyesha nia yake ya dhati ya kuboresha Sekta ya Afya kwa Vitendo, Ili kuwa na jamii yenye Afya bora kwani mikakati kama hii ya kuwa na Wahudumu wa Afya Ngazi ya Jamii itachochea upatikanaji wa Huduma Muhimu za Afya na Elimu ya Afya karibu zaidi na Jamii.

**ASANTENI KWA KUNISIKILIZA**

Mhe. Jenista Mhagama (Mb)

**WAZIRI WA AFYA**